# SHERIA YA MAREKEBISHO YA SHERIA YA KUANZISHA OFISI YA MUFTI NAM. 9 YA 2001

---

## MPANGILIO WA VIFUNGU


| VIFUNGU | MAELEZO |
| --- | --- |
| | **SEHEMU YA KWANZA**<br>**MASHARTI YA AWALI** |
| 1. | Jina fupi na kuanza kutumika. |
| 2. | Kusomwa. |
| | **SEHEMU YA PILI**<br>**MAREKEBISHO YA VIFUNGU** |
| 3. | Marekebisho ya kifungu cha 2. |
| 4. | Kuongezwa kwa kifungu kipya cha 4A. |
| 5. | Marekebisho ya kifungu cha 5. |
| 6. | Marekebisho ya kifungu cha 7. |
| 7. | Marekebisho ya kifungu cha 8. |
| 8. | Marekebisho ya kifungu cha 9. |
| 9. | Marekebisho ya kifungu cha 10. |
| 10. | Kuongezwa kwa kifungu kipya cha 11A. |
| 11. | Kuongezwa kwa kifungu kipya cha 11B. |
| 12. | Marekebisho ya kifungu cha 11. |
| 13. | Marekebisho ya kifungu cha 14. |
| 14. | Marekebisho ya Sheria ya Wakfu na Mali ya Amana, Nam. 2 ya 2007. |

**SHERIA NAM. 8 YA 2019**

**NIMESAINI**

**{DKT. ALI MOHAMED SHEIN}**
**RAIS WA ZANZIBAR NA MWENYEKITI**
**WA BARAZA LA MAPINDUZI**

30 Disemba, 2019

## SHERIA YA MAREKEBISHO YA SHERIA YA KUANZISHA OFISI YA MUFTI NAM. 9 YA 2001

---

**IMETUNGWA** na Baraza la Wawakilishi la Zanzibar.

## SEHEMU YA KWANZA
## MASHARTI YA AWALI

*Jina fupi na kuanza kutumika.*

**1.** Sheria hii itajulikana kama Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Kuanzisha Ofisi ya Mufti, 2019 na itaanza kutumika mara baada ya kutiwa saini na Rais.

*Kusomwa.*

**2.** Sheria hii itasomwa pamoja na Sheria ya Kuanzisha Ofisi ya Mufti Nam. 9 ya 2001, ambapo katika Sheria hii itajulikana kama "Sheria Mama".

## SEHEMU YA PILI
## MAREKEBISHO YA VIFUNGU

*Marekebisho ya kifungu cha 2.*

**3.** Kifungu cha 2 cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa kuongezwa ufafanuzi wa maneno mpya kwa mpangilio wa herufi kama ifuatavyo:

"Baraza" maana yake ni Baraza la Ulamaa Zanzibar lililoanzishwa chini ya kifungu cha 11A (1) cha Sheria hii;

"Madrasa" maana yake ni taasisi ya elimu inayotoa maelekezo kuhusu masomo ya kiislamu ikiwemo Qur an, utamaduni wa Kiislamu (Sunna na Hadithi) za Mtume (S.A.W), Falsafa ya Sheria (Fiqhi) na Sheria za Kiislamu.

Kuongezwa kwa kifungu kipya cha 4A.

**4.** Sheria Mama inarekebishwa kwa kuongezwa kifungu kipya cha 4A mara baada ya kifungu cha 3 kama ifuatavyo:

Muhuri na Nembo ya Ofisi.

"4A.-(1) Kutakuwa na muhuri na nembo ya Ofisi ya Mufti ambayo umbo na ukubwa wake utakuwa kama itakavyoamuliwa na Baraza.

(2) Matumizi ya muhuri na nembo ya Ofisi ya Mufti juu ya waraka wowote yatathibitishwa kwa saini ya Katibu wa Mufti au ofisa mwengine yeyote aliyeidhinishwa na Katibu wa Mufti.

(3) Waraka wowote ili uwe ni hati iliyotolewa na Ofisi ya Mufti, utatakiwa kuwekwa muhuri wa Ofisi ya Mufti na kuthibitishwa kwa mujibu wa kifungu kidogo cha (2) cha kifungu hiki."

Marekebisho ya kifungu cha 5.

**5.** Kifungu cha 5 cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa kuongezwa kifungu kipya kidogo cha (3) mara baada ya kifungu kidogo cha (2) kama ifuatavyo:

"(3) Endapo Mufti atakuwa hayupo, Naibu Mufti atatekeleza kazi na uwezo wote wa Mufti."

Marekebisho ya kifungu cha 7.

**6.** Kifungu cha 7 cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa kufutwa kifungu kidogo cha (2) na kuandikwa upya kama ifuatavyo:

"(2) Mtu atakuwa na sifa za kuteuliwa kuwa Katibu wa Mufti ikiwa mtu huyo:

(a) ni Mzanzibari;

(b) ana angalau shahada ya kwanza katika masuala ya Kiislamu;

(c) ana uzoefu wa angalau miaka minne katika masuala ya utawala wa umma; na

(d) anaheshimika."

Marekebisho ya kifungu cha 8.

**7.** Kifungu cha 8 cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa:

(a) kufutwa kifungu kidogo cha (1) na badala yake kuwekwa kifungu kidogo kipya cha (1) kama ifuatavyo:

"(1) Mufti, kwa kushauriana na Waziri, anaweza kuanzisha idara na vitengo vya Ofisi ya Mufti endapo itahitajika kwa mujibu wa masharti ya Sheria ya Utumishi wa Umma;"

(b) kuongezwa vifungu vidogo vipya vya (2) na (3) mara baada ya kifungu kidogo cha (1) kama ifuatavyo:

(2) Wakuu wa idara zilizoanzishwa katika kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, watateuliwa na Mufti kwa kushauriana na Waziri kwa kuzingatia masharti ya Sheria ya Utumishi wa Umma.

(3) Wakuu wa vitengo watateuliwa na Mufti kwa kuzingatia masharti ya Sheria ya Utumishi wa Umma."

(c) kupanga upya vifungu vidogo vya (2) na (3) vya kifungu hiki kuwa vifungu vidogo vya (4) na (5) kwa mpangilio.

Marekebisho ya kifungu cha 9.

**8.** Kifungu cha 9 cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa:

(a) kuongezwa maneno "Madrasa na" baina ya maneno "yote" na "misikiti" yaliyopo katika aya ya (i) ya kifungu kidogo cha (1).

(b) kuongezwa aya mpya za (o) na (p) mara baada aya ya (n) kama ifuatavyo:

"(o) kuratibu Sala za Iddi na Baraza la Iddi;

(p) kusimamia shahada za kuslimu."

(c) kupanga upya aya za (o) na (p) za kifungu kidogo cha (1) kuwa aya (q) na (r) kwa mpangilio.

Marekebisho ya kifungu cha 10.

**9.** Kifungu cha 10 cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa:

(a) kuongezwa aya mpya ya (d) mara baada aya ya (c) kama ifuatavyo:

"(d) kufuta kibali chochote cha mambo ya kiislamu au mkusanyiko wowote wa kiislamu Zanzibar au kumsimamisha mhadhiri wa kiislamu ambaye atakiuka masharti ya kibali hicho."

(b) kupanga upya aya ya (d) na (e) za kifungu kidogo cha (1) kuwa aya (e) na (f) kwa mpangilio.

Kuongezwa kwa kifungu kipya cha 11A.

**10.** Sheria Mama inarekebishwa kwa kuongezwa kifungu kipya cha 11A mara baada ya kifungu cha 10 kama ifuatavyo:

Uanzishwaji wa Baraza la Ulamaa.

"11A-(1) Kunaanzishwa chombo cha kumshauri Mufti kitakachojulikana kama Baraza la Ulamaa Zanzibar.

(2) Baraza litaundwa na:

(a) Mufti ambaye atakuwa Mwenyekiti wa Baraza;

(b) Kadhi Mkuu;

(c) Naibu Mufti;

(d) Naibu Kadhi Mkuu;

(e) Katibu Mtendaji wa Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana;

(f) Mkuu wa Chuo cha Kiislamu cha Serikali; na

(g) Sheikh mmoja kutoka kila wilaya.

(3) Isipokuwa mwenyekiti na wajumbe wanaoingia kwa nafasi zao, wajumbe waliotajwa chini ya aya ya (g) ya kifungu kidogo cha (2) cha kifungu hiki, watateuliwa na Waziri kwa kushauriana na Mufti kulingana na uzoefu, elimu na taaluma inayohusiana na mambo ya kiislamu.

(4) Katibu wa Mufti ndiye atakayekuwa Katibu wa Baraza.

(5) Utaratibu wa mikutano, muda wa wajumbe, maslahi ya wajumbe na mambo mengine ya uendeshaji wa mikutano ya Baraza yataainishwa na Kanuni zilizotungwa chini ya Sheria hii."

Kuongezwa kwa kifungu kipya cha 11B.

**11.** Sheria Mama inarekebishwa kwa kuongezwa kifungu kipya cha 11B mara baada ya kifungu cha 11A kama ifuatavyo:

Kazi za Baraza.

"11B.-(1) Baraza litamshauri Mufti juu ya masuala ya kiislamu yaliyowasilishwa kwake kwa madhumuni ya kutolewa fat-wa na litafanya kazi nyengine yoyote kama itakavyoamuliwa na Mufti;

(2) Maamuzi ya Mufti baada ya kupata ushauri wa Baraza katika kutowa fat-wa yatakuwa ndiyo maamuzi ya mwisho."

Marekebisho ya kifungu cha 11.

**12.** Kifungu cha 11 cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa kufutwa aya ya (a) na kuweka badala yake aya mpya ya (a) kama ifuatavyo:

"(a) fedha zinazoidhinishwa na Baraza la Wawakilishi kwa njia ya ruzuku."

Marekebisho ya kifungu cha 14.

**13.** Kifungu cha 14 cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa:

(a) kufutwa maneno "Laki Moja" na kuwekwa badala yake maneno "Laki Mbili" katika kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki.

(b) kufutwa maneno "Laki Mbili" na kuwekwa badala yake maneno "Laki Tano" katika kifungu kidogo cha (2) cha kifungu hiki.

Marekebisho ya Sheria ya Wakfu na Mali ya Amana Nam. 2 ya 2007.

**14.** Sheria ya Wakfu na Mali ya Amana Nam. 2 ya 2007 inarekebishwa kwa kufutwa aya ya (d) ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu cha 4.

**UMEPITISHWA** na Baraza la Wawakilishi la Zanzibar, tarehe 27 Novemba, 2019.

..............................................

(RAYA ISSA MSELLEM)

***Katibu wa Baraza la Wawakilishi la Zanzibar.***